Tutakuja pamoja!

Tarehe 16/09/2017 - Maandamano dhidi ya ubaguzi wa rangi
Carneval ya jamii - Berlin

Tuko wengi, wengi zaidi kuliko tunavyofikiri. Wiki moja kabla ya uchaguzi mkuu tunataka kujionyesha hadharani na kupaza sauti zetu. Tunataka kusimulia hadithi zetu za ukimbizi na namna tulivyopokonywa haki zetu, uzoefu wetu kwenye ofisi za mamlaka ya mji na ubaguzi wa rangi tuliopitia, pia kuhusu kukaribishwa na kubaki hapa. Tutakuja pamoja: Kwa siasa yenye umoja. Pamoja kwa ajili ya wote - tutakutana tarehe 16/09/2017 mjini Berlin!

Maandamano yataanza tarehe 16/09/2017 saa saba mchana mbele ya Wizara ya Mambo ya Ndani Berlin (karibu na kituo kikuu cha treni). Mahali pa mkutano wa mwisho ni “Oranienplatz”.

Maandamano hayo yataundwa kwa magari tofauti yaliyobeba mabango yenye mada tofauti: kupinga kufukuzwa nchini, kudai haki ya elimu kwa kila mtu, kuhimiza miji yenye umoja na kadhalika. Kutakuwa na hotuba, muziki na kila kitu mnachokuja nacho – kwa mfano hadithi, picha au ishara. Kitu pekee tunachotaka kuacha nyumbani ni bendera za kitaifa kwa sababu maandamano hayo yanahusu haki sawa kwa kila mtu bila kujali anatoka wapi.

Je, tutasafiri vipi kwenda Berlin?
Watu wote wanaotaka kuhudhuria kwenye maandamano haya mjini Berlin watasafirishwa kwa mabasi Jumamosi asubuhi! Watachukuliwa mbele ya au karibu na makazi ya wakimbizi (Lager)!

Ili tuwahi kufika saa tano asubuhi kwenye kambi ya maandalizi ya carneval Berlin, mabasi yataondoka mapema. Baada ya kujiandikisha na kununua tiketi, punde tutawapatia taarifa zaidi kuhusu wakati wa kuondoka kwa mabasi hayo. Kwa hiyo, tafadhali hakikisheni mnatupatia nambari zenu za simu za ukweli wakati mnapojiandikisha.

Bei ya amana ya tiketi moja ni Euro tano. Mtarudishiwa pesa hiyo mkionyesha tiketi zenu mkiwa kwenye basi kwenda Berlin.

Mtu ambaye ameshanunua tiketi au anayependa kununua tiketi au aliye na maswali yeyote yanayohusu ununuzi wa tiketi, anaweza kupiga simu au kutuma ujumbe kwa njia ya Whatsapp kwenye namba ifuatayo: 01575 – 5290998.

Tutawapigia simu kabla safari haijaanza ili kuwaambia mabasi yataondoka lini na wapi. Mabasi hayo yatawarudisha kwenye makazi yenu tena baada ya maandamano kuisha. Kwa hiyo msisahau kubeba chakula na vinywaji! :)

Vitu vya kubeba:
Kitambulisho, vinywaji na madawa mnayotumia mara kwa mara.

Taarifa za kisheria kwa ajili ya maandamano ya tarehe 16/09/2017
Nchini Ujerumani kila mtu ana haki ya kuhudhuria maandamano. Hiyo imeruhusiwa. Kama mtu anahudhuria au hahudhurii maandamano hiyo haina umuhimu katika utaratibu wa kupewa hifadhi nchini. Watu ambao wanakwenda kwenye maandamano hawana nafasi ndogo kwenye utaratibu wa kutambuliwa nchini.

Lakini inawezekana kwamba polisi watakagua vitambulisho vya waandamanaji kwenye

SWAHILI

Berlin, 16.9.2017

11:00 | PREPARATION CAMP |
MINISTRY OF INTERIOR, ALT-MOABIT 140, CLOSE TO HAUPTBAHNHOF
13:00 | PARADE | MINISTRY OF INTERIOR TO ORANIENPLATZ

maandamano hayo. Kwa hiyo kila mtu ni sharti aje na kitambulisho chake (kwa mfano kibali cha makazi, ruhusa ya kipekee kwa kubaki (Duldung), BüMa, n.k.).

Pengine hakutakuwa na shida yeyote na polisi kwenye maandamano. Hata hivyo tutawapatia namba ya simu mkiwa kwenye mabasi. Mnaweza kuipigia namba hiyo ya simu kama mkiwa na shida na polisi. Kwa kutumia namba hiyo mtaweza kuongea na mwanasheria. Lakini sisi tunaamini kwamba hakutakuwa na shida yeyote na polisi.

Je, kila mtu anaruhusiwa kusafiri kwenda Berlin?
Wakimbizi wengi wanayo ruhusa ya kutembea kwa uhuru nchini Ujerumani. Wanaweza kusafiri kila mahali. Kama ukisafiri kwa siku moja tu kwa ajili ya maandamano, si lazima kuiambia ofisi ya uhamiaji (Ausländerbehörde), . Lakini ukitaka kubaki mjini Berlin kwa zaidi ya siku mbili, inabidi kuwaambia wafanyakazi wa huduma za jamii kwenye makazi yenu.

Lakini kuna wakimbizi wale walio na *Residenzpflicht*; yaani wanaolazimika kubaki kwenye jimbo, wilaya au mji wanapoishi. Hao hawana ruhusa ya kusafiri kila mahali nchini Ujerumani.

Baadhi ya wakimibizi wenye *Residenzpflicht:*
- wale walio katika miezi yao mitatu ya kwanza Ujerumani
- au wakiwa bado wanaishi katika kambi ya kwanza.

Zaidi ya hayo inawezekana kwamba mtu ana *Residenzpflicht*
- kama alikuwa na matatizo na polisi au ofisi ya uhamiaji (Ausländerbehörde)
- au kama kuna uwezekano kwamba atafukuzwa nchini hivi karibuni.

Kwa kawaida ofisi za uhamiaji (Ausländerbehörde) huandika ndani ya kitambulisho cha mtu mwenye *Residenzpflicht* kwamba hana haki ya kutembea huru nchini na haruhusiwi kusafiri kila mahali.

Kwa kesi hii, utaona imeandikwa kwenye kitambulisho: “Räumliche Beschränkung”.

Yule ambaye ana *Residenzpflicht* na anapenda kusafiri kwenda Berlin ili kuhudhuria kwenye maandamano, anaweza kuwasiliana nasi. Halafu tutashauriana kama hata hivyo inawezekana kusafiri kwenda Berlin.

Kwa hali yeyote tutakuwa watu wengi na hiyo ndiyo itatupa nguvu. Jiungeni na marafiki ili kuunda kundi. Kisha mtaweza kujadiliana ni nini mtakachofanya katika hali gani. Na kama bado mna maswali, mnaweza kutupigia simu.

V.i.S.d.P.: Carni Valla, Straße der Pariser Kommune 13, 10356 Berlin